: swahili
Informasjon til asylsøkere i Norge

NOAS

MAELEZO

KWA WAOMBAJI WAUKIMBIZI - NORWAY

Brosha hiki kimetayarishwa na Shirika la wakimbizi (NOAS).
NOAS ni shirika la haki ya kibinadamu ambalo sio la kiserikali. Noas ni shirika ambalo hutoa maelezo na usaidizi wa kisheria kwa wakimbizi.

Brosha hii ina maelezo muhimu kwako wewe unayeomba ukimbizi na unayehitaji hifadhi nchini Norway.

HAPA UNAWEZA KUSOMA KUHUSU:

- Ni nani ambaye ana haki ya hifadhi?
- Ni nani anayeweza kupewa kibali cha kuishi nchini kwa sababu za kibinadamu?
- Ni nchi gani ambayo itashughulikia ombi lako la ukimbizi?
- Ni nani atashughulikia ombi lako la ukimbizi nchini Norway?
- Nini kitafanyika wakati umeomba hifadhi?
- Ushauri muhimu kuhusu mahojiano ya ukimbizi?
- Wajibu na haki zako kama mwombaji wa ukimbizi?
- Kiapo cha siri

1. NANI AMBAYE ANA HAKI YA HIFADHI?

Una haki ya hifadhi, kwa maana nyingine una haki ya ukimbizi, iwapo uko kwenye hatari ya kuuwawa, kuteswa, ama kunyanyaswa kwa aina nyingine ukirudi kwenye nchi yako ya asili.
Ikiwa serekali ya nchi yako ya asili inaweza kukulinda ama kama kuna nafasi ya usalama mahali pengine ndani ya inchi yako ya asili, kwa kawaida hutakuwa na haki ya hifadhi nchini Norway.

Nani ambaye ana haki ya hifadhi, inafwatana na makubaliano ya kimataifa ambayo nchi ya Norway ina lazimishwa kutimiza.

2. NI NANI ANAYEWEZA KUPEWA KIBALI CHA KUISHI NCHINI KWA SABABU ZA KIBINADAMU?

Ikiwa huna haki ya hifadhi, serikali itachunguza kama unatimiza mashariti ya kupewa makao kwa sababu zenye uzito za mahitaji ya kibinadamu ama kwa sababu maalum za uhusiano wako na Norway. Hiki kinaitwa kibali cha kuishi nchini kwa sababu za kibinadamu.

Kwa kawaida ni lazima uwe na paspoti ya inchi yako ili upewe kibali cha kuishi . Kama hujapeana paspoti yako kwa serikali inaweza kusababisha ombi lako likataliwe au upewe kibali ambacho hakikupi haki ya kudumu ya kuishi ama kuungana na familia yako.

3. NI NCHI GANI AMBAYO ITASHUGHULIKIA OMBI LAKO LA UKIMBIZI?

Sio wote ambao wanaoomba ukimbizi Norway ambao ombi lao hushughulikiwa hapa. Ushirikiano wa Dublin ni ushirikiano kati ya nchi za Europa ambao unamaanisha kwamba maombi ya muombaji wa ukimbizi yanaweza kushughulikiwa kwenye nchi mojawapo ya hizo tu.

Ombi lako laweza kushughulikiwa katika nchi nyingine inayohusishwa kwenye uhusiano wa Dublin, iwapo katika nchi hio:

- Umeandikishwa kwa alama ya vidole.
- Umeomba ukimbizi
- Umepewa visa au kibali cha makao
- Unafamilia ya karibu

Kwa kawaida inachukua miezi miwili au sita kwa serikali ya Norway kuchunguza na kuamua kama unapashwa kuhamishiwa nchi nyingine.

Iwapo unahitaji maelezo zaidi, unaweza kupata kijitabu chenye habari zaidi kuhusu ushirikiano wa Dublin kutoka NOAS.

4. NI NANI HUSHUGHULIKIA MAOMBI YAKO YA UKIMBIZI NCHINI NORWAY?

Idara ya Uhamiaji (UDI) ni sehemu ya serikali ya Norway. Watumishi wa Idara ya uhamiaji watakuhoji na kuamua kama utapewa makao. UDI huangalia maombi yote kwa makini na kushughulikia kila ombi peke yake.

5. NI UTARATIBU GANI UNAOFUATWA UKIOMBA UKIMBIZI?

Unajiandikisha kama muombaji ukimbizi kwa Polisi
Polisi anakuchukua picha yako na alama za vidole vyako. Watakuuliza ujitambulishe na uelezee jinsi ulivyosafiri mpaka Norway. UDI watakuuliza kuhusu sababu zako za kuomba hifadhi. Ikiwa una vitambulisho, itakubidi uvipeane unapojiandikisha.

Utahamishiwa kwenye kituo chamda cha kupokea wakimbizi
Baada ya kujiandikisha, utapelekwa kwenye kituo cha mapokezi. Utakaa hapo kwa siku chache kabla ya kupelekwa katika kituo kingine cha mda au cha kawaida. Watumishi wa kituo hicho watakupatia maelezo zaidi kuhusu wajibu na haki zako kwenye kituo.

Utapimwa Kifua kikuu
Katika siku za mwanzo kituoni utapimwa kifua kikuu. Kupimwa ni lazima kwa watu wote. Ikiwa una tatizo kubwa la afya linalohitaji matunzo ya haraka, unapaswa kufahamisha kituo cha huduma ya afya.

Utapewa maelezo na uongozi kutoka kwa NOAS
Katika siku zako za mwanzo katika kituo cha mapokezi, utapokea maelezo kutoka kwa NOAS. NOAS ni shirika la haki za binadamu lisilo la kiserikali, ambalo hushughulikia haki za wakimbizi nchini Norway. Wajibu wa NOAS katika kituo cha mapokezi ni kutoa maelezo na ushauri kwa wakimbizi. Utaonyeshwa sinema au filamu yenye maelezo kuhusu utaratibu wa kuomba ukimbizi na pia utazungumza na mfanyakazi wa NOAS. Nia ya mazungumzo hayo ni kukutayarisha kwa maulizo ya UDI kuhusu ukimbizi.
Ni muhimu kutumia mazungumzo hayo kwa kuuliza maswali yoyote unayoweza kuwa nayo kuhusu namna ya kuomba ukimbizi. Mazungumzo hayo yatafanyika kwa lugha unayoifahamu vizuri.

Iwapo kuna uwezekano kuwa utahamishiwa nchi ingine ya Ulaya kulingana na ushirikiano wa Dublin, ni muhimu ueleze ili uhakikishe kwamba umepokea maelezo sahihi. Wafanyakazi wa NOAS wamekula kiapo cha siri.

Utahojiwa na UDI
Kwenye mahojiano kuhusu maombi ya ukumbizi ndio nafasi yako muhimu yakueleza sababu zako za kuomba hifadhi.. Mahojiano ya ukimbizi kwa kawaida yanachukuwa masaa mengi. Eleza kwa uthabiti na kikamilifu mambo uliyopitia na ni nini unachoogopa kama utarudishwa tena nchini mwako. Kutakuwa na kalimani wakati wa mahojionao. Mkalimani huyo amekula kiapo cha kuweka siri na hapendelei upande wowote. Iwapo una matatizo ya kuelewa yanayosemwa, unapaswa umfahamishe muulizaji mara moja. Mwishoni mwa mahojiano , utaweka sahihi kwenye ripoti kuhusu yale ambayo yamesemwa wakati wa mahojiano. Mkalimani atakusomea maelezo hayo. Ikiwa unapenda kubadilisha kitu chochote kwenye ripoti hiyo, lazima useme kabla ya kuweka sahihi.

Utahamishiwa kwenye kituo cha mapokezi cha kawaida ambapo utaishi ukingojea majibu kutoka kwa UDI
Kuishi kwenye kituo cha mapokezi ni bure. Ukipenda, unaweza kuishi kibinafsi wakati unapongojea majibu kutoka kwa UDI, lakini ukifanya hivyo hutapokea msaada wowote wa kifedha. Na ukihamia makao mengine ni lazima uripoti kwa kituo cha mapokezi ili wajuwe anwani yako mpya. Ni muhimu anwani yako mpya isajiliwe ili majibu kutoka kwa UDI yaweze kukufikia.

Habari mpya
Ukipata habari mpya ambazo ni muhimu kwa ombi lako la ukimbizi baada ya mahojiano, unapaswa kujulisha UDI mara moja. Eleza kwa nini hukueleza hyao kwenye mahojiano. Wafanyakazi wa kituo unachoishi wanaweza kukuelezea jinsi ya kufikisha harari hizo.

Unasubiri majibu kutoka kwa UDI
UDI inaweza kuchukua kutoka wiki kadhaa hadi zaidi ya mwaka kushughulikia ombi lako. Ikichukua mda mrefu, inaweza kuwa ni kwa sababu UDI lazima ifanye uchunguzi ili kuhakikisha kwamba yale maelezo uliyotoa ni sahihi. Inawezekana pia kuwa ni kwa sababu UDI inachunguza hali katika nchi yako asili, au kwa sababu kuna watu wengine wengi wanaosubiri majibu kutoka kwa UDI.

Utapata majibu kutoka kwa UDI: Kibali cha makao au kukataliwa

Kibali cha makao
Ukipewa kibali cha makao, utapewa pia ruhusa ya kuishi ndani ya manispaa/kummune fulani. Utapokea maelezo zaidi katika kituo cha mapokezi.

Kukataliwa
Ikiwa ombi lako limekataliwa, una haki ya kulalamika. Utapewa mwanasheria bure, kwa kawaida ndani ya ma saa matano, atakayekusaidia kuandika malalamiko. Ni lazima ulalamike katika muda wa wiki tatu, kuanzia tarehe umeliopata majibu.
Kwa kawaida unakubaliwa kukaa nchini Norway wakati malalamiko yako yanaangaliwa, lakini hutakubaliwe kukaa nchini ikiwa UDI inaamini kuwa ombi lako wazi wazi halina sababu za msingi.

Mahakama ya uhamiaji (UNE)
UNE ndiyo huangalia malalamiko yako. UNE inaweza kukuita kwa mkutano au kukuuliza utume maelezo zaidi.

Ombi lako likikataliwa, ni wajibu wako kurudi kwenye nchi yako ya asili
Ni lazima urudi nyumbani kabla ya muda wako wa mwisho uliotolewa na polisi kuisha, kwa kawaida huwa unapewa wiki mbili. Baada ya muda huo wa mwisho kupita, hauna haki ya kisheria ya kuishi nchini Norway.
Ukipata katalio la mwisho, kumaanisha kwamba UNE inakubaliana na uamuzi wa UDI wa kukataa ombi lako la ukimbizi, unaweza kuchagua kurudi kwa hiari yako kwa msaada wa Shirika la Kimataifa la uhamiaji (IOM), au kusindikizwa nje ya nchi na polisi (kurudishwa kwa nguvu).

Kurudi kwa hiari na IOM
Serikali ya Norway inahakikisha kwamba kuna uwezekano wa kurudi nyumbani kwa hiari yako. Kurudi kwa hiari kunamaanisha kuwa utashirikiana kutayarisha safari yako ya kurudi nyumbani kwa kutoa ombi kwa mpango wa kurudi kwa hiari unaoitwa Mpango wa Usaidizi wa Kurudi kwa Hiari (VARP).

Mpango huo wa VARP ni ushirikiano kati ya UDI na IOM, wanaopanga safari yako ya kurudi nyumbani. Ukirudi kwa hiari yako, ni serikali ya Norway inalipa safari yako ya kurudi.

Wote ambao hawana kibali cha makao nchini Norway wanaweza kutuma ombi la kurudi kwa hiari. Iwapo ombi la ukimbizi limekataliwa, una muda mfupi wa kuondoka Norway. Kama unapenda kurudi kwa hiari, unapaswa kutuma ombi lako kwa IOM muda mfupi baada ya ombi lako la ukimbizi kukataliwa. IOM ikikubali ombi lako utapatiwa ushauri na

msaada wa kutafuta vitambulisho vya usafiri na tikiti. Ili uweze kusafiri na IOM, ni lazima uwe na paspoti halali au hati/vitambulisho vya kusafiri vilivyotolewa na serikali ya nchi yako ya asili. Iwapo hauna paspotii halali au hati ya kusafiri, IOM itakusaidia kuomba hati hio kutoka kwa ubalozi wa nchi yako ulio karibu. IOM itakusaidia katika safari yako na pia ukifika katika nchi yako ya asili, kama unataka.

Unaweza kupata habari zaidi kuhusu kurudi kwa hiari na usaidizi wa kujaza fomu ya ombi katika kituo cha mapokezi, ofisi za mkoa za UDI au IOM.

Kurudishwa kwa nguvu
Ikiwa baada ya maombi yako kukataliwa mara ya mwisho hurudi nyumbani kwa hiari, utasindikizwa nje ya nchi na polisi baada ya siku ya mwisho ya kuondoka kupita.

Ni lazima wewe mwenyewe sasa ulipe matumizi ya kusindikizwa kutoka nje ya nchi. Kama huna uwezo wa kulipa tiketi ya ndege, serikali italipa safari yote, lakini utawajibika kulipa gharama hio. Usipolipa gharama hio ya kusindikishwa kwako unaweza kukataliwa visa ya kuingia nchini Norway na nchi zingine za Ulaya wakati wa baadaye.

Ukifanya vitendo vya uhalifu
Ukifanya vitendo vya uhalifu, ombi lako la ukimbizi litaangaliwa kwa haraka zaidi, ili uweze kutolewa nchini Norway.Ukifanya jambo lolote kinyume cha sheria, unaweza pia kufukuzwa kutoka Norway, jambo ambalo lina maana ya kuwa hutaweza kuingia tena Norway na nchi zingine nyingi za Ulaya.

6. USHAURI MUHIMU KUHUSU MAHOJIANO YA UKIMBIZI

- Elezea waziwazi na kikamilifu sababu zilizokufanya utoke katika nchi yako ya asili na ni kitu gani unachoogopa kitatokea kama utarudi.
- Sisitiza kwa yale wewe mwenyewe umepitia na yale ambayo yatakutokezea iwapo itakubidi urudi.
- Eleza kwa usahihi kiasi iwezekanavyo.
- Kama una watoto ambao wako chini ya umri wa miaka 18, elezea hali yao na waliyoyapitia.
- Uliza muulizaji akueleze iwapo kuna jambo lolote usiloelewa.
- Iwapo una hati za lazima ambazo zinahusiana na ombi lako la ukimbizi unapaswa uzibebe unapoenda kwenye mahojiano.
- Elezea ukweli. Ukitoa maelezo ambayo sio sahihi inaweza kusababisha kukataliwa kwa ombi lako la ukimbizi. Matokeo yake unaweza kufukuzwa kutoka nchini Norway na kufanya ukataliwe kuingia tena Norway na nchi nyingi za Ulaya.

Wanawake wanaoomba ukimbizi
Wanawake wanaweza kuwa wamenyanyaswa kwa jinsi tofauti na wanaume. Kwa hivyo inaweza kuwa vigumu kwao kuelezea kuhusu waliyoyapitia hasa kwa wanaume. Kama unapenda unaweza kuzungumza na mfanyakazi wa kike wa NOAS. Fahamisha NOAS haraka iwezekanavyo ukishatazama sinema ya maelezo.
Siku ya mahojiano na UDI unaweza pia kuomba mhoji na makalimani wa kike.. Unaweza kutoa ombi hilo wakati wa mazungumzo yako na NOAS.

Umekuja pamoja na watoto wenye umri wa chini ya miaka 18?
Hali ya mtoto ni muhimu katika kutathmini sababu za kuomba ukimbizi. UDI atapenda kujua kama mtoto ana sababu zake binafsi za kuomba ukimbizi na jinsi mtoto peke yake anaangalia hali yake ya maisha. Ni muhimu kuelezea UDI kuhusu hayo yote wakati wa mahojiano ya kuomba ukimbizi.

UDI inafanya mazungumzo na mtoto wenye umri zaidi ya miaka saba. Ni muhimu mtoto apate fursa ya kujielezea kwa maneno yake mwenyewe yale ambayo ameyapitia. Mara nyingi watoto wanayahisi matatizo kwa uchungu zaidi kuliko kuliko watu wazima. UDI haizungumzi na mtoto kama mtoto mwenyewe hataki.

7. WAJIBU NA HAKI ZAKO KAMA MUOMBAJI WA UKIMBIZI

Una wajibu wa kushirikiana inapohusu kujitambulisha
Ni muhimu kwa serikali ya Norway kujua wewe ni nani. Kwa hivyo ni muhimu upatiane hati ambayo inaweza kuthibitisha wewe ni nani.

Iwapo unanyanyaswa na serikali ya nchi yako ya asili, serikali ya Norway haitakulazimisha uwasiliane na serekali ya inchi yako ili upate vitabulisho.

Kama serikali ya Norway ina shaka kuhusu kujitambulisha kwako, una hatari ya:
- Kutokuaminika
- Kupunguza uwezekano wa kupewa makao/ukimbizi
- Kupoteza haki ambazo ungelipatiwa
- Kupewa kibali cha makao chenye ufinyu.

Una wajibu wa kutoa maelezo sahihi
Kama anayeomba ukimbizi, ni lazima ueleze sababu za kuomba hifadhi.
Kwa hivyo ni lazima ujitahidi unavyoweza kushirikiana na kutoa hati zinazohitajika.
Bila kujali uliyoyasikia kutoka kwa wengine kabla ya kutoa ombi la ukimbizi, ni muhimu uelezee kwa serikali ya Norway ukweli kuhusu sababu zako peke yako za kuomba ukimbizi. Ni hatia ya jinai kutoa maelezo yasiyo sahihi. Inaweza pia kusababisha kufukuzwa nchini.

Una haki ya kufanya kazi unapoomba ukimbizi
Unaweza kupewa kibali cha kufanya kazi unaposubiri ombi lako lishughulikiwe mradi tu uwe unawezakutoa hati za kujitambulisha na huko kwenye utaratibu wa Dublin. Kibali cha kazi ni cha mda wa miezi sita lakini kinaweza kuombwa upya.

Una haki ya kutibiwa
Una haki ya kupata matibabu unayohitaji unapongojea ombi lako likamilike. Matibabu kwa watoto chini ya umri wa miaka 12 hufanywa bila malipo. Watu wazima kwa kawaida lazima watoe mchango kiasi fulani kwa matibabu. Ikiwa unahitaji usaidizi kutoka kwa mwanasaikolojia, unaweza kutoa ombi kwa UDI ili wakulipie gharama yako. Kwa maelezeo zaidi, wasiliana na wafanyakazi wa kituo cha mapokezi. Iwapo una matatizo makubwa ya kiafya, unapaswa kufahamisha UDI.

Unaweza kuondoa ombi lako la ukimbizi
Unaweza kuondoa ombi lako la ukimbizi wakati wowote. Baada ya kufanya hivyo unaweza kuomba IOM ikusaidie kusafiri nyumbani.

8. KIAPO CHA SIRI
Polisi, UDI, UNE, mkalimani, mwanasheria, watumishi wa afya na NOAS wana wajibu wa kuhifadhi siri. Hii inamaanisha kuwa hawawezi ktuoa habari kuhusu ombi lako la ukimbizi kwa serikali ya nchi yako ya asili.
Hawawezi pia kueleza uliyoyasema kwa watu ambao hawashughulikii ombi lako la ukimbizi. Ni kinyume cha sheria kuvunja kiapo cha siri. Kwa hivyo usiogope kujielezea kikamilifu kuhusu sababu zako za kuomba ukimbizi.

ANWANI

IDARA YA UHAMIAJI YA POLISI (POLITIETS UTLENDINGSENHET)

Polisi huandikisha na kusajili wakimbizi wapya.
Polisi pia hurejesha wakimbizi ambao hawaondoki nchini Norway kwa hiari yao punde maombi yao ya ukimbizi yamekataliwa mara ya mwisho.

Anwani ya Posta: Postboks 8102 Dep., NO-0032 Oslo, Norway
Anwani ya kuzuru: Christian Krohgs gate 32, 0186 Oslo
Simu.: + 47 22 34 24 00, Faksi: + 47 22 34 24 80
Barua pepe: pu@politiet.no

IDARA YA UHAMIAJI (UDI)

Ni taasisi ya serikali ambayo wajibu wake ni miongoni mwa mengine mengi kuangalia maombi ya ukimbizi, visa, uraia , na kuunganisha familia tena. UDI pia wana jukumu la kuongoza vituo vya kupokea wakimbizi.

Anwani ya Posta: Postboks 8108 Dep., NO-0032 Oslo, Norway
Anwani ya kuzuru: Hausmannsgt. 21, 0182 Oslo
Simu.: + 47 23 35 15 00, Faksi: + 47 23 35 15 01
Tovuti: www.udi.no, Barua pepe: ots@udi.no

SHIRIKA LA KIMATAIFA LA UHAMIAJI (IOM)

Maelezo ya usaidizi wa kurudi kihiari

Anwani ya Posta: Postboks 8927 Youngstorget, NO-0028 Oslo, Norwe
Anwani ya kuzuru: Storgata 10a, sakafu/etg ya 2, 0155 Oslo
Simu.: + 47 23 10 53 20, Faksi: + 47 23 10 53 21
Barua pepe: osloreturn@iom.int

Saa za kufungua: Siku ya Juma: 10:00 – 15:00, Wikendi: Kumefungwa

MAHAKAMA YA UHAMIAJI (UTLENDINGSNEMNDA - UNE)

Ni kikundi cha utawala kinachofanya kazi kama mahakama ya kuangalia rufaa/malalamiko yanayotokana uamuzi wa kukataliwa kwa maombi ya makao na UDI.

Anwani ya Posta: Postboks 8165 Dep., NO-0034 Oslo, Norway
Anwani ya kuzuru: Stenersgt. 1B/C, 0050 Oslo
Simu.: + 47 21 08 50 00, Faksi: + 47 21 08 50 01
Tovuti: www.une.no, Barua pepe: postmottak@une.no

SHIRIKA LA MSALABA MWEKUNDU, NORWAY (NORGES RØDE KORS)

Huduma za utafutaji, husaidia waliofika nchini Norway kutafuta na kuwasiliana na wale waliotengana nao kutokana na vita, mapambano, na majanga.
Msalaba mwekundu hautoi maelezo yako kwa UDI au wengine.
Huduma hiyo ni bila malipo.

Anwani ya Posta: Postboks 1 - Grønland, NO-0133 Oslo, Norway
Anwani ya kuzuru: Hausmannsgt. 7, 0186 Oslo
Simu.: + 47 22 05 40 00
Tovuti: www.rodekors.no, Barua pepe: tracing@redcross.no

NOAS ni shirika la haki ya kibinadamu ambalo sio la kiserikali. Noas ni shirika ambalo hutoa maelezo na usaidizi wa kisheria kwa wakimbizi.

Brosha hii ina maelezo muhimu kwako wewe unayeomba ukimbizi na unayehitaji hifadhi nchini Norway.

Shirika la wakimbizi (NOAS)
Anwani ya Posta: Torggata 22, 0183 Oslo
Anwani ya kuzuru: Postboks 8893 Youngstotget., 0028 Oslo
Simu.: +47 22 36 56 60, Faksi: +47 22 36 56 61
Tovuti: www.noas.org, Barua pepe: noas@noas.org